# Ukweli wa Ubaguzi wa rangi, Unyanyasaji na Kashfa

**Racial Discrimination, Harassment and Hatred - Swahili**

## Nini maana ya ubaguzi wa rangi?

Ubaguzi kwa ujumla hutokea pale mtu anapotendewa visivyo sawa ukilinganisha na utendewavyo mtu mwingine katika mazingira yaleyale au sawa kutokana na wasifu wa mtu huyo

Katika sheria za Australia ni uvunjaji wa sheria kumbagua mtu katika hali mbalimbali , ikijumuisha asili, rangi, jinsia, umri, wasifu wa kindoa ulemavu na dini au imani za kisiasa.

Ubaguzi huangaliwa katika njia kuu mbili:

**Ubaguzi wa moja kwa moja**: Ambapo mtu hutendewa vibaya sana kuliko mtu mwingine kwa sababu tu ya wasifu fulani.

**Ubaguzi usio wa moja kwa moja**: Ambapo kanuni mahitaji au mazoea ambayo hutumika kwa kila mmoja sawa yatakuwa na madhala kwa sehemu kubwa ya watu wenye wasifu Fulani.

## Nini ubaguzi wa rangi kinyume cha sheria?

Kwa wewe ili uwe na malalamiko juu ya ubaguzi wa rangi, kitendo kinacholalamikiwa lazima kiwe cha uvunjaji sheria.

Ni uvunjaji sheria kwa mtu au shirika kukubagua katika hali ya asili ya rangi, utaifa, kuzoa au ukabila.

Ubaguzi huu lazima uwa umefanyika katika mazingira ya umma kama vile ajira, elimu, kufikia katika sehemu za umma na kutumia magari ya umma, wakati wa kununua bidhaa au huduma au malazi ya umma. Kwamfano huwezi kuzuiliwa kuingia katika jengo la umma kutokana na asili yako.

Kuna mipaka juu ya hili na unatakiwa kupata ushauri kujua kuwa mipaka hiyo inaendana na mazingira yako. Kwa mfano, siyo kinyume cha sheria kwa mtu kumbagua mtu mwingine kiasili kama mtu anayebaguliwa amaajiliwa kufanya kazi kama msaidizi wa watoto katika nyumba ya mtu mwingine.

## Nini Unyanyasaji wa rangi?

Ni kinyume cha sheria kumnyanyasa mtu kutokana na asili yake, rangi, ukoo, kabila au utaifa katika mazingira ya umma kama vile kazini, elimu na malazi.

Unyanyasaji wa kiasili unaweza kuchukua mifumo mingi ukijumuisha vitisho, matusi na kuelemea katika asili ya mtu rangi, uzao, kabila au asili ya taifa.

## Nini kashfa za kiasili?

Sheria za Australia zinapinga marufuku kashfa za asili. Kashfa za asili hutokea wakati mtu anapofanya, kusema au huzusha kitu katika umma ambacho kina pelekea kumudhalilisha mtu mwingine kutokana tu na rangi, uasili, utaifa au ukabila wake.

Hata hivyo kunautofauti katika sheria hii na utapaswa kupata msaada / ushauri wa kisheria kuweza kubaini utofauti endapo utahusiana na swala lako.

KANUSHO: Maelezo ya karatasi hii yanatoa mwongozo wa jumla tu na yasitumiwe badala ya ushauri wa kisheria. Kwa kiwango cha juu kinachoruhusiwa na sheria, CASE kwa wakimbizi Inc. inakanusha hasara yoyote ya moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja itakayompata msomaji ikihusiana na kutegemea au kuhusiana na maelekezo katika karatasi hii. Msomajai lazima apate ushauri wa kisherai kutokana na mazingingira yake binafsi.

Kufungua malalamiko juu ya ubaguzi wa rangi, unyanyasaji wa rangi au kashfa ya rangi

Kunasheria za jumuiya ya madola na zile za dola ambazo huhusika na ubaguzi wa kiasili, unyanyasaji na utoaji kashfa. *Sheria ya jumuiya ya madola ya ubaguzi wa rangi ya mwaka 1975* ambapo malalamiko yote ya sheria hii kwa kawaida yatawakilishwa katika tume ya haki za binadamu. Sheria ya Australia Magharibi ni ile ya *Fulsa sawa sheria ya 1984 (WA)* na malalamiko yote chini ya sheria hii hutumiwa kwenye tume ya fursa sawa

Mara nyingi unaweza kufanya uchunguzi endapo ungependa malalamiko yako yashughulikiwe chini ya sheria ya za jumuiya ya madola au sheria za nchi.

Kwa ujumla lalamiko kwa yeyote kati ya tume hizo lazima litumwe ndani ya miezi 12 tangu tukio la mwisho la ubaguzi.

Mara baada ya kutuma lalamiko kwa yeyote kati ya jumuiya ya madola au tume ya taifa, tume itaamua endapo ichunguze hatua ya kwanza itumike kwa mhusika kuitwa kwenye mkutano wa usuluhishi.''Usuluhishi'' ni mchakato ambapo tume huhusisha pande zote katika mazungumzo ya suala na kujaribu kufikia suluhisho. Wewe utapendekeza ni aina gani ya suluhu ungependelea kwa mfano, msamaha wa wazi wa maandishi.

## Wapi pa kupata msaada

CASE kwa wakimbizi inc. ni taasisi isiyo ya kiserikali na sio ya kidini ambayo inasaidia wahamiaji na shughuli zote za kisheria katika mila na isimu ya Lugha(Cald)katika jamii ya Australia magharibi. CASE kwa wakimbizi inc. inaweza kukusaidia kufanya malalamiko kwenye kamishna ya haki za binadamu au kamishna ya haki sawa kwa wote.

Huduma zote sio za malipo, ingawa misaada ya watu binafsi na mashirika inapokelewa kwa ukarimu. Michango yote ya zaidi ya AUD $2.00 haina vati.

Mawasiliano ya CASE kwa wakimbizi inc.ni haya yafuatayo :

145 Stirling Street, Perth
Western Australia 6000

Simu:(08) 92277311

Kinukushi: (08) 92277188

Email:admin@caseforrefugees.org.au

KANUSHO: Maelezo ya karatasi hii yanatoa mwongozo wa jumla tu na yasitumiwe badala ya ushauri wa kisheria. Kwa kiwango cha juu kinachoruhusiwa na sheria, CASE kwa wakimbizi Inc. inakanusha hasara yoyote ya moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja itakayompata msomaji ikihusiana na kutegemea au kuhusiana na maelekezo katika karatasi hii. Msomajai lazima apate ushauri wa kisherai kutokana na mazingingira yake binafsi.